



KUZUIA WADUDU Toleo, TPC 10

Mende wa Epilachi

(Mexican bean beetle, *Epilachna varivestis*)

Aina ya jamii hii ya mende ni kati ya ile idadi ndogo ya mende wanaotafuna majani. Jamii hii imesamba katika Amerika ya Kati na Kusini, Afrika na bara Hindi.

Mahasimu

Jamii hii ya mende huhisimu mimea ya vibweta-kunde kama vile maharagwe, maharagwe ya lima, kunde, soya, mahindi, malenge, viazi na mbilingani.

Dalili

Wadudu wachanga hutafuna chini ya majani. Wadudu waliokomaa hutafuna majani na sehemu changa za mmea na hata maua na mbegu.

Kutambua

Mdudu aliyekomaa hufanana na *ladybird (Coccinellidae)*, ila tuu tabia ya malisho ndiyo hutofautiana. Rangi yake ni manjano na wekundu kwa mbali. Gamba linalofunika mabawa lina madoa (mabatobato) kumi na sita (16). Mdudu anaweza kuwa wa urefu wa 6 hadi 8mm na unene wa 4 hadi 6mm.

Kizazi

Mayai ya rangi ya manjano hutagwa chini ya jani. Mayai huangua baada ya siku 4 hadi 5. Vijidudu vilivyoanguliwa ni rangi ya manjano na urefu wa 8mm. Miili ya vijidudu hao hugawanywa katika sehemu iliyo na vinywele 4 au 6. Wakati wa baridi vinywele hivi ni vyeusi. Vijidudu hao hujishikilia kwa kutumia vinywele hivyo hadi kukomaa na kuanza kutafuna majani.

Kuzuia na Kukabili

Utunzi bora: Iwapo wadudu wataonekana, Ng'oa mimea iliyoadhiriwa na kuchoma au kuchimbia chini kiasi cha 15cm ili kuua vijidudu wachanga.

Dawa za Kunyunyiza

Mwarobaini (*Azadirachta indica*): Mti huu ulitokea sehemu za India, Mwarobaini umesambaa sehemu nyingi za dunia kama bara Hindi na Afrika. Mbegu zaweza kupatikana kwa urahisi. Mbegu huokotwa kisha kukaushwa. Wakati unapohitaji kutayarisha dawa, utapondaponda mbegu hizo kisha kulowesha kwa siku moja. Tumia 2 hadi 50g ya unga wa mbegu kwa lita moja ya maji. Nyunyiza mchanganyiko huu kwenye mimea iliyoadhiriwa

Mkurubuku (*Derris elliptica*, *D. malaccensis*, *D. uliginosa*): Mmea huu ulitokea sehemu za nyanda ya chini ya Malay Archipelago. Kata mizizi ya upana wa 2 hadi 6cm kisha kukatakata vipande vya urefu wa 5cm. Pondaponda kisha kuongeza sabuni kidogo na maji. Chuja mchanganyiko huo na kufifisha kisha kutumia mara moja. Tumia kiasi cha 1Sabuni: 4 mizizi: 225 maji.

Pareto (*Chrysanthemum cinerariaefolium*): Maua ya pareto yanayo kemikali iliyo na uwezo wa kuua wadudu. Mmea wa pareto hufanya vyema katika sehemu zenye muinuko wa 1600m, na pia sehemu zisizo tumika kwa kikamilifu. Mmea huu haufanyi vyema katika sehemu zilizo na rutuba nyingi, kwani sumu hufifia.

Chuna maua wakati wa mchana. Kausha kwenye jua. Iwapo utaweka kwa muda mrefu, kausha kisha kuweka mahali pakavu na pasipo na mwangaza. Mwangaza hufufisha ukali wa sumu.

Dawa ya pareto: Changanya 20g ya pareto na lita 10 za maji. Sio lazima kuongeza sabuni. Tumia mara moja kwa kunyunyiza.

Aina ya maharagwe ya kiaziki kuu (*Yam bean, Pachyrrhizus erosus*): Kusanya mbegu zilizokomaa. Mbegu hizi ni sumu.

Siaga 65g ya mbegu kisha kuchanganya na lita 12 za maji. Nyunyizia mimea iliyoadhiriwa.

Kitunguu Saumu (*Allium sativum*): Kitunguu saumu hutumiwa kwa matumizi ya kila aina kama vile kuangamiza wadudu, vimelea, minyoo na hata kuangamiza kupe.

Dawa ya Kitunguu Saumu: Loweka vitunguu vitatu kwenye mafuta ya taa kwa siku mbili. Ongeza kijiko kimoja cha sabuni na lita 10 za maji. Tumia mara moja kabla ya nguvu kufifia.

Kumbuka: Dawa zote zapaswa kunyunyizwa kabla ya mayai kutagwa

This update: Jan 2005

Tafsiri na: **Patrick Bunyali Kamoyani, September 2004. Maragoli Kenya.**

Email pbkamoyani@lycos.co.uk or pbkamoyani@excite.com

Tel +254-(0)-721 612 607

HDRA- Kwa huduma za kilimo hai, Ryton Organic Gardens Coventry, CV8 3LG, UK
Simu +44 (0)24 7630 3517 Kipepesi +44 (0)24 7663 9229 Barua pepe: ove-enquiry@hdra.org.uk
Mtandao: <http://www.hdra.org.uk>

Makala haya ni mkusanyiko wa utafiti wa kisayansi na maarifa ya kilimo hai. Maelezo haya sio bayana na viwango vya kimataifa kuhusu kilimo hai. Maelezo ya ziada kuhusu mbinu za kilimo hai yaweza kupatikana kutoka kwa HDRA. Waweza kunakili makala haya kwa sababu zisizo za kifaida. Shukrani ni kwa Charlton Community Development Trust kwa mchango wa kutayarisha makala haya.